
# NASIKIA KUITWA



Pastor James Kalekwa

# NASIKIA KUITWA.

James Kalekwa

Orodha ya Yaliyomo

Tabaruku ........................................ 4

Salamu na Utangulizi ........................................ 5

SURA YA KWANZA: ........................................ 7

UHITAJI WA KIONGOZI KWENYE SWALA LA WITO NA UTUMISHI. ........................................ 7

SURA YA PILI: ........................................ 14

KIONGOZI HUNIFAA VIPI NINAPOSIKIA WITO? ........ 14

SURA YA TATU: ........................................ 21

UTENDAJI WA MUNGU DUNIANI ........................................ 21

SURA YA NNE: ........................................ 33

NAMNA GANI YA KUJUA KWAMBA MUNGU ANANIITA. ........................................ 33

SURA YA TANO: ........................................ 45

JE, NINI SIO WITO? ........................................ 45

SURA YA SITA: MKAZO KUHUSU WITO (UTUMISHI) 48

SURA YA SABA: ........................................ 54

VIZUIZI HIVYO NI KAMA ........................................ 54

Kuhusu Mwandishi: ........................................ 58

Kuhusu New Vine Church: ........................................ 58

Mawasiliano na Mwandishi: .....**Error! Bookmark not defined.**

## Tabaruku

Mfululizo wa vitabu hivi vya kieltroniki (e-books) bure kwa kila atakaye; ni himizo la kiungu ndani yangu kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.

Ninatabaruku kitabu hiki kwa kanisa la Kristo na kwa nchi yangu niipendayo, Tanzania.

Kanisa litashinda na kushamiri zaidi!

Tanzania, ninakupenda kwa moyo wote!

## Salamu na Utangulizi

Mfululizo huu wa vitabu vya kieletroniki ni maono ambayo Mungu ameweka ndani ya mtumishi wake, mume wangu mpenzi, kama namna yake ya kuonyesha shukurani kwa Mungu kwa zawadi ya maisha.

Ninamfahamu mume wangu kama mtu anayempenda Mungu kupitiliza. Yuko tayari kulipia gharama yoyote ile kuonyesha hilo. Ni mtu anayewapenda watu wa Mungu kwa namna ambayo sijawahi kuona. Yamekuwa ni maombi yake kuyagusa maisha ya wengi kwa kadiri inavyowezekana kabla Yesu Kristo hajarudi.

Anapoadhimisha siku ya kuzaliwa kwake **Juni 20**, amekuandikia kitabu hiki, akapangilia na kufanya kipatikane kwako bila malipo yoyote. Nimemwona anavyokesha; wakati mwingine kuamka alfajiri sana au kuchelewa sana kulala ili kukamilisha uandishi. Nimemuona anavyoomba na kuombea wasomaji, anavyojisomea na kutafiti ili kuhakikisha anafanya uwasilishaji wa thamani.

Ningependa tuthamini zawadi hii ambayo sisi wengine tunanufaika nayo bila kulipia gharama:

1. Mshukuru Mungu pamoja nasi kwa zawadi hii ya maisha ya Pastor James Kalekwa kisha muombee maisha marefu na afya njema.
2. Mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumpongeza ukisema ni kwa namna gani

huduma yake imeyagusa maisha yako. Ninajua hili litaufurahisha sana moyo wake.

3. Wafikishie vitabu hivi walau watu hamsini tu. Ni vitabu vinatolewa bila malipo (vimeyagharimu maisha ya mwandishi ili vikufikie).
4. Usiuze vitabu hivi. Tuligundua kuwa kuna watu wanavisambaza kwa malipo ya fedha. Hiyo si sawa. Itakuwa ni kwa hasara yako mwenyewe ukifanya hivyo.

Baada ya kuyasema hayo, nikuhakikishie ya kwamba mtu huyu mkuu wa Mungu amejaa hekima za kiungu na neno ambalo siku zote hutokeza shuhuda maishani mwa wengi. Kwa kusoma kitabu hiki, ushuhuda wako unafuatia. Nikutakie usomaji mwema.

Na heri ya kuzaliwa kwa mpendwa wetu, zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu, Pastor JK.

Frida James Kalekwa (Mama Pastor JK)
Mke wa mwandishi
Juni, 2024
Dodoma, Tanzania

# SURA YA KWANZA:

# UHITAJI WA KIONGOZI KWENYE SWALA LA WITO NA UTUMISHI.

Wito siku zote huja na vitu vingi ndani yake. Huja na moto mifupani, hisia kali, huruma kwa makundi fulani ya watu au maeneo fulani, usongo wa kuyarukia mambo na kuanza kumletea Bwana matokeo, hukausha hamu ya mambo mengine yote ya kimaisha na kutaka utumishi tu.

Hivyo namna wito unavyokuja unalazimu (necessitate) mambo mengi kwa ajili ya kuhakiksha kwamba kila kilichofungamanishwa na wito huo kinatokezwa. Moja ya jambo la msingi ambalo wito huliita kwa nguvu zaidi ni uwepo uongozi. Uongozi au maongozi yana nguvu kubwa ya namna gani wito uende, maongozi yana nguvu ya kuukuza wito huo na hata kuudidimiza. Maomngozi huulea wito mpaka utokeze na kuwa jambo jema la manufaa. Kukosekana kwa maongozi hasa nyakati wito unachemka ndani ya mtu, huwa ni jambo la hatari sana.

Nitataka sana tusome andiko hili  la 1 Samweli 3:1-10. Ni msitari mingi kiasi lakini ni salama zaidi kusoma neno la Mungu. Sababu mojawapo kwanini huwa ninaambatanisha maandiko kwenye machapisho yangu ni ili mtu aweze kusoma mara hiyo tu na kuchunguza, kuona mikazo na kufuata vizuri uwasilishaji wangu baada ya andiko husika. Ninakusihi katika jina la Yesu Kristo usome mistari yote ninayoiambatanisha hapa:

*"Basi, mtoto Samweli akamtumikia BWANA mbele ya Eli. Na neno la BWANA lilikuwa adimu siku zile; hapakuwa na mafunuo dhahiri. 2Ikawa wakati huo, Eli alipokuwa amelala mahali pake (tena macho yake yalikuwa yameanza kupofuka, hata asiweze kuona), 3na taa ya Mungu ilikuwa haijazimika bado, na Samweli alikuwa amelala katika hekalu la BWANA, palipokuwa na sanduku la Mungu; 4basi, wakati huo BWANA akamwita Samweli; naye akasema, Mimi hapa. 5Akamwendea Eli kwa haraka, akasema, Mimi hapa; kwa maana uliniita. Akasema, Sikukuita; kalale tena. Naye akaenda, akalala tena. 6BWANA akaita mara ya pili, Samweli! Samweli! Akaondoka akamwendea Eli,*

*akasema, Mimi hapa; kwa maana uliniita. Akajibu, Sikukuita, mwanangu; kalale tena. 7Basi Samweli alikuwa hamjui BWANA bado, na neno la BWANA lilikuwa bado halijafunuliwa kwake. 8BWANA akamwita Samweli mara ya tatu. Naye akaondoka akamwendea Eli, akasema, Mimi hapa; kwa maana uliniita. Ndipo Eli akatambua ya kuwa BWANA ndiye aliyemwita yule mtoto. 9Kwa hivyo Eli akamwambia Samweli, Enenda, kalale; itakuwa, akikuita, utasema, Nena, BWANA; kwa kuwa mtumishi wako anasikia. Basi Samweli akaenda akalala mahali pake. 10BWANA akaja, akasimama, akaita vile vile kama kwanza, Samweli! Samweli! Ndipo Samweli akasema, Nena, BWANA; kwa kuwa mtumishi wako anasikia."*

Kutokea kwenye mfano wa Samweli na Eli kuna mengi ya kujifunza hapa. Kama mwitika-wito ni dhahiri kuwa unahitaji mtu wa kutoa msaada wa kupambanua sauti ya Mungu katikati ya sauti nyingi; Kuitofautisha sauti ya BWANA na ile ya Eli mtumishi wake. Unaona zinafanana na inafikia hatua Samweli hawezi kutofautisha ipi ni sauti ya Mungu. Kuichanganya sauti

ya Mungu na sauti nyinginezo hasa nyakati ambazo wito unawaka moto ndani yako ni jambo la kufikia tu kama usiposaidika vyema na waliokutangulia.

Ninaposema kupambanua sauti ya Mungu kutoka kwenye sauti nyingi ninamaanisha kutenganisha hisia, mihemko ndani ya moyo au hali ya maisha au maono ya watu yanayoendelea kwa ujumla wake na wito.

Kuna wakati unaweza kudhani umeitwa kumbe ni mihemko ya ndani na hisia zinazoendelea ndani na hii inahusisha kuitikia WITO wa sauti binafsi au sauti za watu wengine. Kuna namna maalum ya kuitika sauti ya Bwana na hupaswi kuitika sauti nyingine zozote kabisa na hii inatokea kwenye ufahamu wa sauti ya Bwana na utambuzi wake.

Umeona vyema kwenye hilo andiko ya kwamba Samweli alikuwa analala hekaluni… mahali ambapo sanduku la Bwana lipo. Ninataka kufikiri ya kwamba kijana alikuwa anampenda Mungu na ana shauku na mambo ya Mungu kwa ukubwa huo. Halafu angalia wapi alikuwa amelala Eli "Mahali pake" Hiyo ni

kukuonyesha ya kuwa kulikuwa na sehemu maalum za kulala kuhani kwenye hekalu. Lakini Samweli hakuwa huko. Shauku inakula ndani yake!

Taarifa ya zaidi tunayopewa kuhusu mzee Eli ni kwamba, "*tena macho yake yalikuwa yameanza kupofuka, hata asiweze kuona"*. Yaani upande mmoja tuna mzee, mwenye uono dhaifu, amelala mahali pake (hata siyo kwenye hekalu mahala pa sanduku la Bwana). Kwa lugha ya sasa hivi ungeweza kumdhania ni mzee aliyepoa kiroho au amerudi nyuma au haelewi *"dynamics"* za mambo ya kiroho. Upande mwingine, tuna kijana ambaye amejawa na shauku kumuhusu Mungu kiasi cha kulala mahali pa sanduku la Bwana. Sauti ya Mungu ilivyoanza kuita ndiyo utagundua umuhimu wa maongozi ya waliokutangulia. Na kama Eli angekuwa na wivu… wengi huwa wanshtuka nikisema hivyo. Ndiyo alipaswa kuwa na wivu kwanini Bwana anamwita Samweli na si watoto wake Eli wa kibaiolojia. Unaelewa? Sasa kama angekuwa na wivu, angempotosha kijana. Ashukuriwe Mungu kwa ajili ya Eli. Unaona ya kwamba mzee hakukurupuka bali

aliihakiki kiasi cha kujiridhisha ya kwamba hiyo ni sauti ya Bwana.

Tutazame ni kwanini anayeitwa anapaswa kuitikia wito mapema. Hapa ninazungumzia swala la kuitika tu kwanza simaanishi kwenda au kuchukua hatua yoyote. Kuitika ni kukubali na kuupokea mwito na kuanza kuyaelekeza maisha yako huko… Kuitika ni kufika mahali pa kujua, "Sina maisha mengine isipokuwa maisha ya utumishi tu!" Wengi sana huenda… huanza utekelezaji kabla ya kuitika.

i. Kulelewa wito mapema inaongeza tija kwenye ufalme wa Bwana. Itakua heri kwa wanufaika wa wito wako na wewe pamoja na watu wanaokuhusu.

ii. Kuitika wito na kuuelewa hupunguza mahangaiko ya maisha. Unaona ile hali ya kuchanganyikiwa aliyoipata Samweli… fikiria ndiyo inakuwa hali endelevu maishani mwako?

iii. Kuelewa wito mapema utaishinda hofu (woga) na dhana potofu zinazosemwa kuhusu utumishi. Ufahamu huu ni muhimu sana kwamba maswali

mengi kuhusu maisha hujibiwa baada ya kuitika wito, hivyo kila aina ya hofu juu ya maisha na utumishi hukomeshwa na hukatwa kabisa wakati huu.

iv. Ukielewa wito mapema utajiandaa na kupangilia mapema kwenye utumishi na maisha kwa ujumla. Kuelewa mapema kunasaidia utumishi kutoibuka kama ajali na hivyo matokeo yote yatakuja kwa mpangilio uliowekwa mapema kabisa.

v. Kuelewa wito mapema hukupa kutumika muda mrefu kwenye ufalme wa Mungu kwa wakati wa maisha yote.

vi. Kuelewa wito mapema inatoa nafasi ya kuwafikia watu wengi sana duniani.

vii. Kuelewa wito mapema inasaidia kuzidisha matokeo mapema na makubwa kwenye maisha yako.

viii. Kuelewa wito mapema hutoa zawadi ya kuishi na kuona matunda ya kazi yako.

# SURA YA PILI:

# KIONGOZI HUNIFAA VIPI NINAPOSIKIA WITO?

Kiongozi huyu ni yule anayetoa msaada wa namna ya kuelewa na kusikia wito ndani ya mwamini. Sasa, ni nini kazi zake kuhakikisha kuwa wito unatokeza ndani ya mwamini? Muda wote hapa tutachota mifano kutoka kwenye simuliz yetu nanga ya Eli na Samweli.

i. Kuweka mazingira ya utambuzi wa wito wa Bwana. Tazama mfano wa Eli (kiongozi) na Samweli (mwitika-wito). Kiongozi mzuri hawezi kukuita bali mazingira anayoyatengeneza ni yale yanakukutanisha na Mungu kwa kutumia eneo ambalo umeitwa na kutokea hapo wito huibuka.

ii. Kukusaidia kuelewa viashiria vya wito wa Bwana maishani mwako. Kwenye muktadha wa andiko letu nanga, utagundua ya kwamba sauti ya Bwana ilikuwa adimu kwenye zama hizo. Ni ngumu kudhania ya kwamba alikuwa ni Bwana

anamuita… inawezekana kijana alikuwa anaota ndoto au ana fikra zake. Lakini Mzee Eli alivyoona jambo hili linakuja kwa kujirudia-rudia, akagundua hiyo inaashiria ya kwamba kijana anaitwa na Mungu. Hii si ndoto ya usiku au *insomnia* tu!

iii. Kufundisha kwa undani namna ya kuitikia wito ndani yako. Unaona ni jinsi gani Eli alimsaidia Samweli mpaka maneno ya kusema kuitika sauti ya Bwana iliyokuwa ikimuita? Anaweza kukusaidia mambo gani ufanye na namna gani ufanye ili kurahisisha zoezi lako la la kuitika wito wa Mungu maisha mwako. Ni kweli Samweli alikuwa anaitwa na Mungu lakini alikuwa hajui namna ya kuitika… Nimeona vijana kadhaa wakirabikiwa baada ya moto kuwaka mifupani mwao na wao wakatafsiri ni ishara ya kwenda. Kumbe ni moto unawaka ili waitike na kupokea maelekezo kutoka kwa Bwana. Bahati mbaya sana wakaenda umbali mrefu bila kuwa na

maelekezo. Kwa taarifa yako, kuna namna ya kuitika!

iv. Kufundisha hatua za awali za kuchukua baada ya kusikia wito na kuitika. Si unajua Mungu anaweza akakuita sasa ili akutume baada ya miaka mitano kutokea sasa? Swali, muda huu ambao anakuita mpaka muda wa kwenda ufike utakuwa unafanya nini?

Ukisoma kitabu nimeandika kinaitwa **"Kazi ya Mungu ni Kazi"** nimefafanua madaraja mawili ambayo watu wanaitiwa: a). Waasisi wa huduma b). Wasaidizi wa huduma (waendelezaji)… Na hapa haimaanishi ubora au udhaifu bali ni namna ya Mungu ya kuita na kuendesha kazi yake yeye mwenyewe.

Sasa, kwa kila daraja kuna mambo mahususi ya kufanya ili uweze kutumika kwa uaminifu kwenye eneo ambalo Mungu amekuitia. Kumbuka kipimo cha Mungu cha namna gani tumemtumikia ni uaminifu: Vyema mtumwa mwema na ***mwaminifu***! Uaminifu ni kufanya kile umeagizwa kufanya… kubaki hapo.

Ili uweze kujiandaa vyema na kwa uhakika unahitaji mtu aliyekutangulia akusaidie namna ya kuyaendea yote hayo:

- Nini unatakiwa kufanya
- Vitabu gani unapaswa kusoma
- Watu gani unapaswa kuwasikiliza na kuambatana nao
- Namna ya kuomba
- Mambo ya kushughulika nayo kwenye maisha yako binafsi
- Maswala ya maadili na nidhamu

v. Kufundisha maandalizi ya utumishi kabla ya kuingia kwenye huduma rasmi. Kuna maandilizi mahususi ya kiutumishi ambayo unapaswa kuyafanya kabla haujaingia kutekeleza ule wito unaousikia ukiwaka kwenye mifupa yako. Kwenye kitabu cha **"Kazi ya Mungu ni Kazi"** nimetambulisha aina sita za kimaandalizi ambazo unatakiwa kufanya… mpaka maandalizi ya kimwili ujue.

vi. Kujenga msingi wa ujasiri na kuweka msukumo wa kushinda hofu ya yasiyokuwepo, yajayo na yasiyojulikana. Kwa sababu ya asili yake, wito siyo kama kipande cha keki. Huwa unavuta maswali mengi sana… maswali ya kila rangi. Na kwa asili, mwanadamu angependa ajibiwe maswali yote kwa wakati mmoja ili achukue hatua za kiutekelezaji. Maswali mengi ni matokeo ya uwezo wa akili ya mwanadamu kuwa na ukomo. Kwa hiyo, hofu huzaliwa. Kuna hofu ni kwa sababu ya kutojua tu… kuna hofu ni kwa sababu ya mambo yajayo. Mpaka uyafikie ndiyo ujionee mwenyewe. Kuna hofu za mambo yasiyokuwepo kabisa. Unahitaji mtu atakayepanda ujasiri ndani yako. La sivyo, unaweza kwenda kwa kujitutumua au kwa kujaribu sana!

vii. Kujenga uwezo ambao utatokeza tija na uamuru matokeo makubwa. Kweli muhimu sana ambayo

nisingependa uikose ni kwamba utumishi una pande mbili pacha: a). Upande wa uungu na b). Upande wa uanadamu – Upande wa uungu ndiyo unazilisha wito, neema, kibali, upako na mambo hayo. Wakati upande wa uanadamu pamoja na mambo mengine unadai uwezo! ni kwamba utumishi, mfano uchungaji, umefungamanishwa na uwezo na ujuzi wa mambo mengi ulio ndani ya mtumishi (Mchungaji). Huwezi kuwa mtumishi mwenye tija sana kama hauna uwezo (capacities). Moja ya uwezo unaotakiwa na Maandiko ni ujuzi wa kufundisha… sasa, tofautisha neema, huduma au karama ya kufundisha – vyovyote vile. Kuna kitu kinaitwa ujuzi wa kufundisha! Kama unao… unao; kama hauna…hauna!

Kuna uwezo wa kusimamia (administration) na kuongoza makundi ya watu, kuratibu mambo mengi kwa wakati mmoja; uwezo wa kubeba hisia zako bila kuathiri kazi ya Mungu (siyo unaumizwa kidogo tu, unaamua kuzira). Huwezi kuwa mtumishi mzuri na *emotional breakdowns*

kama mtoto wa chini ya miaka kumi na mbili. Huo ni uwezo. Utumishi utayataka hayo yote kutoka kwako.

Kazi ya kiongozi wako ni kukujengea uwezo kwa kukufungulia dunia ya utumishi (expose you to the realms of ministry) ujionee mwenyewe.

viii. Kufafanua maswala na kila jukumu ambalo linapaswa kufanywa na mwitika-wito. Kazi nyingine ya kiongozi ni kukuonyesha majukumu ambayo yanapaswa kutimilizwa na wewe; hufafanua maswala (issues) yakuhusuyo

# SURA YA TATU:

# UTENDAJI WA MUNGU DUNIANI

Kuna namna ya Mungu anafanya duniani na namna anayotumia kuyatokeza ni kupitia wanadamu.

*"Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu;* ***wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi.*** *Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba."* Mwanzo 1:26-27

Mungu anaitawala dunia na vyote vilivyomo ndani yake kwa njia ya mwanadamu. Ndiyo maana baada ya anguko, dunia iliathiriwa. Makosa yoyote ya mwanadamu huleta hasara si tu kwa mwanadamu, bali hata kwa uumbaji wote wa Mungu.

Uelewa huu ukiingia ndani yako basi ujasiri utazaliwa ndani yako kuhusu wito na utumishi.

*"Lakini Nuhu akapata neema machoni pa BWANA."* Mwanzo 6:8

*"BWANA akamwambia Nuhu, Ingia wewe na jamaa yako yote katika safina; kwa maana nimekuona wewe u mwenye haki mbele zangu katika kizazi hiki."* Mwanzo 7:1

Mungu anataka kuiangamiza dunia kwa gharika na kuikoa dunia kwa wakati mmoja. Kwa upande kuikoa dunia, alitafuta mtu ili atekeleze kusudio hilo na akampa maelekezo mahususi. Mungu hakushuka kutenda lolote la kiuokozi… Nuhu alitenda! Hakuamchia Mungu kwa sababu Mungu naye alikuwa amemwachia Nuhu.

Unakumbuka wakati Mungu anataka apate kundi fulani jipya la watu duniani ambalo atalitumia kama shamba darasa kuelezea makusudio yake kwa mwanadamu… akamfuata mtu anaitwa Abramu. Akamwita kutoka kwao ili aanze ukoo na hatimaye taifa jipya.

*"BWANA akamwambia Abramu, Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha."* Mwanzo 12:1

Kipindi cha Ibrahimu, Isaka na Yakobo kinaitwa kipindi cha mababa (partriachal era). Kisha wanaingia nchi ya Misri kujisitiri dhidi ya njaa iliyoikumba dunia. Baadaye wanaongezeka na kuwa taifa. Ili watoke kwenye hali ya utumwa, Mungu anaita mtu… huyo mtu anaitwa Musa.

Sasa, ngoja tuangalie andiko ambalo hata mimi lilinisumbua kidogo lakini baada ya kujifunza utendaji wa Mungu ni kupitia watu nilituliza moyo na kukubaliana na kweli ya neno la Mungu:

*"Na **kwa nabii** **BWANA** alimtoa Israeli katika Misri,*

*Na **kwa mkono wa nabii alihifadhiwa**"* Hosea 12:13

Ni BWANA alifanya… sawa! Lakini hakufanya mwenyewe bali alitumia nabii kuwatoa Misri na alitumia mkono wa nabii kuwahifadhi. Mungu hutumia wanadamu wa kawaida kabisa (aliowatia) kuwahifadhi wanadamu. Ruhusu hiyo kweli iingie ndani yako.

Sasa tazama ni kwa jinsi gani Mungu alimuita Musa.

*"BWANA alipoona ya kuwa amegeuka ili atazame, Mungu akamwita kutoka katikati ya kile kijiti, akasema, Musa! Musa! Akasema, Mimi hapa. 5Naye akasema, Usikaribie hapa; vua viatu vyako miguuni mwako; maana mahali hapo unaposimama ni nchi takatifu. 6Tena akasema, Mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo. Musa akaficha uso wake; kwa maana aliogopa kumwangalia Mungu. 7BWANA akasema, Hakika nimeyaona mateso ya watu wangu walioko Misri, nami nimekisikia kilio chao kwa sababu ya wasimamizi wao; maana nayajua maumivu yao; 8nami nimeshuka ili niwaokoe na mikono ya Wamisri, niwapandishe kutoka nchi ile, hata nchi njema, kisha pana; nchi ijaayo maziwa na asali; hata mahali pa Mkanaani, na Mhiti, na Mwamori, na Mperizi, na Mhivi, na Myebusi. 9Basi, tazama, kilio cha wana wa Israeli kimenifikilia; tena nimeyaona hayo mateso ambayo Wamisri wanawatesa. 10Haya, basi, nitakutuma sasa kwa Farao, ili upate kuwatoa watu wangu, hao wana wa Israeli, katika Misri."* Kutoka 3:4-10

Ninataka uone ni kwa jinsi gani Mungu haruhusu watu wake wawe bila kiongozi hapo juu ili kuwasitiri. Baada tu ya kufa Musa, mara moja, Mungu anamuinua Yoshua kuchukua nafasi ya kiuongozi:

*"Musa mtumishi wangu amekufa; haya basi, ondoka, vuka mto huu wa Yordani; wewe na watu hawa wote, mkaende hata nchi niwapayo wana wa Israeli."* Yoshua 1:2

Huwa ninawaambia kanisani nikifundisha ya kwamba moja ya taarifa za msiba zilizowasilishwa kibabe sana ni hii… Musa amekufa. Wakati Yoshua anajiandaa kulia au kupiga yowe, akaambiwa ***"…haya basi, ondoka, vuka mto huu wa Yordani."*** Subiri kwanza Mungu! Kaburi liko wapi? Siku za maombolezo ziko wapi? Mbendera nusu mlingoti iko wapi? Huyu ni kiongozi wa kitaifa. Upande mwingine huwa ninasema hii ni namna ya "kikatili sana" ya kuitwa kumtumikia Mungu- unapewa taarifa ya msiba halafu unapewa na maelekzo ya kutii na kutendea kazi!

Kimsingi, ninataka uone ya kwamba Mungu anataka wale watu wake wavushwe mto… siyo hata wabebwe mgongoni lakini kuna namna anajua hawawezi kuvuka mto wenyewe. Hivi unakumbuka Yoshua anaambiwaje?

*"Uwe hodari na moyo wa ushujaa,* ***maana ni wewe utakayewarithisha watu hawa*** *nchi hii* ***niliyowaapia baba zao ya kwamba nitawapa****."* Yoshua 1:6

Ni kweli Mungu aliwaapia mababa ya kuwa atawapa uzao wao nchi. Angalia kwa umakini ya kwamba inamuhitaji mwanadamu kuwarithisha wanadamu nchi ambayo hata yeye hajawaapia… ameapa Mungu, lakini unarithisha wewe!

Kisha baada ya utawala wa Yoshua, wenye mafanikio na madhaifu, ya kushindwa kuinua mtu anayefuatia. Ndipo kuna kipindi cha waamuzi kinatokeza hapo katikati. Ngoja nikuonyesha jambo fulani kuhusu waamuzi ili uweze kuthamini na kuelewa kwa nini Mungu anataka uchukulie kwa uzito swala la wito:

*“11Wana wa Israeli walifanya yaliyokuwa ni maovu mbele za macho ya BWANA, nao wakawatumikia Mabaali. 12Wakamwacha BWANA, Mungu wa baba zao, aliyewaleta kutoka katika nchi ya Misri, wakafuata miungu mingine, baadhi ya miungu ya watu wale waliokaa karibu nao pande zote, wakajiinamisha mbele yao; wakamkasirisha BWANA, akaghadhibika. 13Wakamwacha BWANA, wakamtumikia Baali na Maashtorethi. 14Hasira ya BWANA ikawaka juu ya Israeli, naye akawatia katika mikono ya watu waliowateka nyara, akawauza na kuwatia katika mikono ya adui zao pande zote; hata wasiweze tena kusimama mbele ya adui zao. 15Kila walikokwenda mkono wa BWANA ulikuwa juu yao kuwatenda mabaya, kama BWANA alivyosema, na kama BWANA alivyowaapia; nao wakafadhaika sana.* ***16Kisha BWANA akawainua waamuzi, waliowaokoa na mikono ya watu hao waliowateka nyara.*** *17Lakini hawakuwasikiliza hao waamuzi wao, maana walifanya uasherati kwa kuifuata miungu mingine, wakajiinamisha mbele yao; wakageuka upesi, na kuiacha njia ile waliyoiendea baba zao, waliozitii amri za BWANA bali*

*wao hawakufanya hivyo.* ***18Na wakati BWANA alipowainulia waamuzi, ndipo BWANA alikuwa pamoja na mwamuzi huyo, akawaokoa na mikono ya adui zao siku zote za mwamuzi huyo; maana BWANA alighairi kwa ajili ya kuugua kwao kwa sababu ya watu wale waliowaonea na kuwasumbua.*** *19Lakini ikawa, wakati alipokufa mwamuzi huyo, wakarudi nyuma wakafanya maovu kuliko baba zao, kwa kuifuata miungu mingine ili kuitumikia, na kuinama mbele yao; hawakuacha matendo yao, wala njia zao za ukaidi.”* Waamuzi 2:11-19

Kuna mduara wa ajabu sana hapo juu ukisoma utashangaa. Ya kwamba, wakibaki peke yao bila mwamuzi wanakuwa kama mahayawani (they go wild). Na wanakuwa kitafunwa chepesi kabisa kwa adui zao. Lakini Mungu akitaka kuwasaidia, anainua mwamuzi na wanakaa salama na akili zinawarudi. Huwa ninapenda kusema, mwanadamu akikosa maongozi ya kiroho huwa hayawani, hafugiki… ni mbaya kuliko mnyama!

Sasa, katikati ya Yoshua na waamuzi kulikuwa na uongozi wa wazee ambao hautolewi taarifa nyingi sana

kwenye Maandiko Mtakatifu (Rejea Waamuzi 1:7). Baada ya kipindi cha waamuzi ambacho kwa ujumla wake kutokea kwa mababa mpaka kwa waamuzi ulikuwa ni utawala unaoongozwa na Mungu mwenyewe – Theokraisia.

Baada ya hapo kinanuka kipindi cha Ufalme ambapo waisraeli wanataka wafalme kama yalivyo mataifa mengine.

*"Ndipo wazee wote wa Israeli wakakutana pamoja, wakamwendea Samweli huko Rama;* ***5wakamwambia, Angalia, wewe umekuwa mzee, na wanao hawaendi katika njia zako; basi, tufanyie mfalme atuamue, mfano wa mataifa yote.*** *6Lakini neno hilo likawa baya machoni pa Samweli, waliposema,* ***Tupe mfalme atuamue****. Naye Samweli akamwomba BWANA.* ***7BWANA akamwambia Samweli, Isikilize sauti ya watu hawa katika kila neno watakalokuambia; kwa maana hawakukukataa wewe, bali wamenikataa mimi, ili nisiwe mfalme juu yao****."* 1 Samweli 8:4-7

Ninachotaka uone kwa kukupatia historia yote namna hii ni kwamba watu wa Mungu hawapaswi kusimama wenyewe bila kifuniko cha kiongozi juu yao. Huu unaonekana kuwa ni ufahamu hata kwa watu wenyewe… wanalilia kuwa ni kiongozi juu yao!

Sasa, kwa ufupi tu, baada ya ombi hilo alipatikana mfalme anaitwa Sauli ambaye alifuatiwa na Daudi kisha Suleimani. Hawa waliitawala Israeli ikiwa kama taifa moja kabila zote kumi na mbili (Israeli United). Ajabu na kweli, kila mmoja alitawala kwa miaka arobaini. Baada ya hapo taifa linapasuka pande mbili – Israeli Kaskazini iliyofahamika kama Israeli na jumla ya kabila kumi na makao yake makuu yalikuwa mji wa Samaria; Wakati Iasraeli Kusini yenye kabila mbili tu ilifahamika kama Yuda na makao yake makuu yakiwa Yerusalemu.

Kipindi hiki cha ufalme kilitawaliwa na ibada ya miungu na masanamu kiasi cha kupelekea kuinuka kwa manabii kuwa kama *"check and balance"* ya kiungu kwa watawala. Mataifa yote mawili yalichukuliwa utumwani/uhamishoni kwa nyakati mbili tofauti na baada ya kurudi (Yuda peke yao) wakawa chini ya

magavana – Zerubabeli, Ezra na Nehemia. Ndivyo Agano la Kale linaisha na kupisha ukurasa mpya wa Agano Jipya. Wanamsubiri mfalme wa kimasihi (messianic king). Yesu Kristo… alipokuja naye alianzisha taifa jipya liitwalo kanisa. Nalo alikusudia liwe chini ya uongozi wa watu wenye wito.

*"Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu;* ***12kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu****, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe;"* Waefeso 4:11-12

Unasikia kuitwa? Ni sawa kabisa… uko mahali sahihi! Watakatifu wanahitaji kukamilishwa ili kazi ya huduma itendeke na ukuaji wa kiroho utokee.

Ninachokisema kwenye sura hii ni kwamba Mungu hutenda kazi kupitia wanadamu. Na huyo mwanadamu ni wewe. Umegundua kuanzia pindi Mungu anawakusanya watu kwenye Agano la Kale mpaka Jipya

kila mara amekusudia kuwalea kupitia mwanadamu mwenzao? Huo ndiyo wito sasa!

# SURA YA NNE:

# NAMNA GANI YA KUJUA KWAMBA MUNGU ANANIITA.

**Dalili 18 ya kwamba Mungu anakuita.**

1) Maono ya wazi

Matendo ya mitume 9:1-9

- Unaweza ona malaika
- Unaweza kumuona Bwana Yesu mwenyewe
- Unaweza kumuona Mchungaji wako/Kiongozi wako
- Unaweza ona watu wakiwa na hali fulani
- Unaweza ona maandishi fulani
- Unaweza ona maeneo au taarifa

2) Ndoto

*Yakobo akakaa katika nchi aliyosafiri baba yake, katika nchi ya Kanaani. Hivi ndivyo vizazi vya Yakobo. Yusufu, aliyekuwa mwenye miaka kumi na saba, alikuwa*

*akichunga kondoo pamoja na ndugu zake; naye alikuwa kijana pamoja na wana wa Bilha, na wana wa Zilpa, wake wa baba yake. Yusufu akamletea baba yao habari zao mbaya. Basi Israeli akampenda Yusufu kuliko wanawe wote, maana ni mwana wa uzee wake, akamfanyia kanzu ndefu. Ndugu zake wakaona ya kuwa baba yao anampenda kuliko ndugu zake wote, wakamchukia, wala hawakuweza kusema naye kwa amani.* Mwanzo 37:1-4

3) Kupitia mazingira

*"Ufunuo aliouona nabii Habakuki. Ee Bwana, nilie hata lini, wewe usitake kusikia? Nakulilia kwa sababu ya udhalimu, ila hutaki kuokoa.* ***Mbona wanionyesha*** *uovu, na kunitazamisha ukaidi? Maana uharibifu na udhalimu u mbele yangu; kunaugomvi, na mashindano yatokea. Kwa sababu hiyo sheria imelegea, wala hukumu haipatikani; kwa maana watu wabaya huwazunguka wenyehaki; kwa sababu hiyo hukumu ikipatikana imepotoka."* Habakuki 1:1-4

Jambo au mazingira yanayokukosesha raha ni kiashiria kwamba Mungu anakuita. Huvuta umakini wako ili uweze kusikiliza taarifa za kina ambazo Bwana anakusemesha.

Ni muhimu kutambua hili: Kwa kadri unavyojua njia nyingi za kumsikia Mungu inamrahisishia kuwasiliana na wewe kwa namna mbalimbali.

4) Sauti ya wazi 1Samweli 3:1-10 – Huu ndiyo mfano nanga wa kitabu hiki. Rejea sura za awali.

5) Shauku takatifu/hamu takatifu/ matamanio matakatifu

*"Ni neno la kuaminiwa; mtu akitaka kazi ya askofu,* ***atamani kazi njema****."* 1Timotheo 3:1 Huoni katazo au kukemewa kwa namna yoyote bali kuna maelekezo ya matarajio ya kazi hiyo ya utumishi. Hakuna mtu anayeweza kutamani kazi ya utumishi kama Roho Mtakatifu ndani yake hayupo. Binafsi, ninaamini si sawa kutamani mambo mengine yote mazuri isipokuwa utumishi. Tunaona ni sawa watoto na vijana wetu

kutamani kuwa marubani, matabibu, walimu, waashi, wanasiasa, wanamichezo… isipokuwa tu utumishi! Hiyo si sawa.

6) Kujua kwa undani, uhakika au ushuhuda. Kuwa na uhakika wa ndani. Unajua bila kuwa na chembe ya mashaka. Unajua kwamba unajua ya kwamba unajua.

7) Moto kwenye mifupa. Hii huambatana na kusikia kufanya kazi ya Mungu ili upate ridhiko la ndani upoe.

*"Nami nikisema, Sitamtaja, wala sitasema tena kwa jina lake; basi, ndipo moyoni mwangu kumekuwamokama moto uwakao, uliofungwa ndani ya mifupa yangu, nami nimechoka kwa kustahimili, wala siwezi kujizuia."* Yeremia 20:9

8) Visa vinavyovuta usikivu au umakini wako.

*"Basi huyo Musa alikuwa akilichunga kundi la Yethro mkwewe, kuhani wa Midiani; akaliongoza kundi nyuma ya jangwa, akafika mpaka mlima wa Mungu, hata*

*Horebu. Malaika wa Bwana akamtokea, katika mwali wa moto uliotoka katikati ya kijiti; akatazama, na kumbe! Kile kijiti kiliwaka moto, nacho kijiti hakikuteketea. Musa akasema, Nitageuka sasa, niyaone maono haya makubwa, na sababu kijiti hiki hakiteketei. Bwana alipoona ya kuwa amegeuka ili atazame, Mungu akamwita kutoka katikati ya kile kijiti, akasema, Musa! Musa! Akasema, Mimi hapa."* Kutoka 3:1-4

Tazama Musa na kichaka cha moto, visa hivi vinavuta umakini kumwelekea Mungu. Utasoma kwa undani kuhusu hilo kwenye kitabu cha **"Maono Haya Makubwa"**

9) Kupoteza ladha au maana ya maisha.

*"Ikawa katika mwezi wa Nisani, mwaka wa ishirini wa mfalme Artashasta, na divai imewekwa mbele yake, nikaishika ile divai, nikampa mfalme. Nami mpaka sasa sikuwa na huzuni mbele ya mfalme wakati wo wote. Basi mfalme akaniambia, Mbona umesikitika uso wako, nawe huna ugonjwa? Nini hii, isipokuwa ni huzuni ya moyo? Ndipo nikaogopa sana."* Nehemia 2:1-2

Kuona kama vile dunia yote imekuwa na rangi moja. Hakuna ladha wala hupati hali ya ridhiko kwenye maisha yako. Kuna kitu cha zaidi ambacho unakihitaji lakini saa hiyo hukijui na unaweza usiwe na maneno mazuri ya kuelezea na kufafanua.

10) Uvuvio wa neno

*“Basi neno la Bwana lilimjia Yona, mwana wa Amitai, kusema”* Yona 1:1

*“neno la Bwana lilimjia Ezekielii, kuhani, mwana wa Buzi, kwa dhahiri, katika nchi ya Wakaldayo, karibu na mto Kebari; na mkono wa Bwana ulikuwa hapo juu yake.”* Ezekieli 1:3

*“Katika mwezi wa nane, mwaka wa pili wa Dario, neno la BWANA lilimjia Zekaria, mwana wa Berekia, mwana wa Ido, nabii, kusema”* Zekaria 1:1,

*“Neno la BWANA lililomjia Yoeli, mwana wa Pethueli.”* Yoeli 1:1

Neno la Mungu linakamata hisia, maamuzi, vionjo, maisha yote yanamezwa na Neno. Kuna nyakati ambazo

unaweza kusoma andiko halafu linatokeza kwako kama vile linadai utimilizwaji kutokea kwako. Linaanza kuushawishi moyo wako kwa kiwango ambacho unaona wewe ndiye utekelezaji wa neno hilo. Hapo siyo tu umesoma neno bali Neno limekuijia.

11) Ushuhuda wa kiongozi au kanisa (call out the called)

*"**Paulo akamtaka huyo afuatane naye,** akamtwaa akamtahiri kwa ajili ya Wayahudi waliokuwako pande zile; kwa maana wote walijua ya kuwa babaye ni Myunani."* Matendo 16:3

Hii inahusisha kuwaita walioitwa na hii hufanywa na watumishi wa Mungu wenye wito tayari. Ninachomaanisha hapa ni kwamba kuna watu ambao wana wito wa Mungu maishani mwao lakini kwa sababu fulani ni ama wanaogopa, hawana ujasiri unaotosheleza kuinuka au wanahitaji tu kushikwa mkono.

Kwenye andiko nililonukuu hapo juu anayezungumziwa ni kijana wa mji wa Listra… ambaye alikuja kuwa moja ya wachungaji wazuri na wenye matokeo. Alichunga

kanisa la Korintho kama msaidizi kisha kupewa kuchunga kanisa korofi la Efeso. Jina lake ni Timotheo. Ukisoma nyaraka zote mbili za Paulo kwenda kwa Timotheo, utabaini ya kwamba tayari alikuwa na wito wa Mungu maishani mwake. Ilihitaji mtu wa aina ya Paulo kuuchomoza wito huo.

12) Moyo kufungamanishwa na "OLE"

Ole kwa tafsiri nyingine ni onyo. Hii inafikia wakati ambao Mungu anaondoa machaguo yote na kuacha jambo moja la utumishi ambalo linapaswa kuzingatiwa.

*“Maana, ijapokuwa naihubiri Injili, sina la kujisifia; maana nimewekewa sharti; **tena ole wangu nisipoihubiri Injili!**”* 1Wakorintho 9:16

13) Kuwa na maswali au mahangaiko ndani ya nafsi kuhusu jamii fulani wakati wengine wanaona iko sawa kabisa.

Hii ni namna ambayo Mungu anakutwika mzigo maalum kwa ajili ya kuushughulikia binafsi na hakuna mwingine ataona jambo hilo.

*"Hanani, mmoja wa ndugu zangu, akanijia, yeye na watu wengine waliotoka Yuda; nami nikawauliza* ***habari za Wayahudi waliopona****, hao watu wa uhamisho waliosalia;* ***na habari za Yerusalemu****. 3Wakaniambia,* ***Watu wa uhamisho, waliosalia huko katika wilaya ile, wamo katika hali ya dhiki nyingi na mashutumu****;* ***tena ukuta wa Yerusalemu umebomolewa****, na malango yake yameteketezwa kwa moto.*Nehemia 1:2-3

14) Milango wazi kwenye maeneo fulani fulani.

*"Paulo akatokewa na maono usiku;* ***alimwona mtu wa Makedonia amesimama, akimsihi, na kumwambia, Vuka, uje Makedonia utusaidie.*** *10Basi alipokwisha kuyaona yale maono, mara tukataka kutoka kwenda Makedonia,* ***kwa kuwa tuliona hakika ya kwamba Mungu ametuita tuwahubiri Habari Njema****."* Matendo ya Mitume 16:9-10

*"kwa maana nimefunguliwa mlango mkubwa wa kufaa sana, na wako wengi wanipingao."* 1Wakorintho 16:9

Uwepo wa milango wazi kwenye maeneo fulani ni pendekezo kwamba Bwana anakuita kwenye eneo husika.

15) Madhihirisho ya utendaji wa karama za Roho Mtakatifu kwenye maisha yako.

Uwezesho wowote wa kiungu ambao Mungu amewekeza ndani ya mwamini ni anatoa taarifa kwamba anakuita eneo hilo.

*"Kisha pana tofauti za kutenda kazi, bali Mungu ni yeye yule azitendaye kazi zote katika wote."* 1Wakorintho 12:6

Huoni ya kwamba utakuwa ni uwekezaji usio na tija kwamba Mungu awekeze karama asizotaka zitumiwe? Kwa mtu asiyetaka atumike?

16) Shauku kuu kwenye mambo ya kiungu na huduma kuliko mwamini wa kawaida.

Mungu anawekeza kiu na njaa kuu kuliko kawaida na hivyo kushindwa kutenda sawa na waamini wengine. Kuwa na mzigo wa kuwahudumia watu kwa injili ya Bwana Yesu, kufundisha, kuombea na kutaka kuiona kazi ya Mungu ikisonga mbele na kuenea.

17) Mawazo endelevu kuhusiana na huduma.

Namna Mungu anaweka mzigo mzito ambao kila wakati inapelekea kutafakari na kufikiria juu ya huduma hii inamaanisha Mungu anakuita eneo hilo.

18) Mtiririko wa maisha

Namna ambavyo maisha yanaenda ni lugha ambayo Mungu anazungumza juu ya wapi unaenda na nini kinaendelea kwenye maisha yako kama mwitika wito. Hii inahusisha kila jambo linalotokea kwenye maisha yako liwe jema au mbaya lina tafsiri juu ya wito.

Hapa utagundua, wewe una matamanio yako, lakini maisha yako ni kama yanaelekezwa uelekeo mwingine usioujua wala wakati mwingine kuutamani.

Ukimuuliza Yusufu mwana wa Yakobo kuwa Je, yale ndiyo maisha aliyoyatamani. Asingekubali. Hata anafika mahali pa uelewa ya kwamba Mungu ndiye anaendesha gari la maisha yetu.

*“**Basi si ninyi mlionipeleka huku, ila Mungu**; naye ameniweka kama baba kwa Farao, na bwana katika nyumba yake yote, na mtawala katika nchi yote ya Misri.”* Mwanzo 45:8

Mwisho mwa picha ndiyo anagundua Mungu ndiye mratibu wa matukio yote ili azalishe alichokuwa amekikusudia.

# SURA YA TANO:

# JE, NINI SIO WITO?

Kutokea hapa tunaweza kuchota mambo ambayo yanatoa taarifa juu ya kinachowaka ndani kuwa sio wito, nayo ni haya,

1) Uasi: Ni vyema kufahamu ya kwamba Mungu siye muasisi wa machafuko na mashindano katika mwili wake.

Kwa mfano: kushindwa kukaa kwenye utaratibu kama inavyotakiwa kwenye nyumba ya Mungu (Soma kitabu cha **Kanisa la Mahala Pamoja**). Na pale ambapo unaelekezwa, unarusha mikono na kuamua kuanza huduma… Huo si wito! Hapa Bwana hajakuita. Hata kama hukubaliani na utaratibu (ambao hapo awali ulikuwa unaukubali), basi kuna namna ya kutokukubaliana kama ndugu katika Kristo Yesu. Na pia, kuna namna ya kuaga kutoka kwenye kanisa la mahala. Usiage kwa sababu misuguano hiyo. Wito haufanani hivyo.

2) Kukosoa kwa nia ya kuharibu au kujivuna.

Kwa mfano, hakuna wito wa kubomoa huduma zingine hasa zile zilizokulea kwa maneno ya ukosoaji hata kama hukubaliani nao kifundisho kwa kiasi gani. Kuna yakati wakosoaji wengi hufanya hivyo ili kujivuna, kulisha kiburi chao na kujiwasilisha kama watu bora. Hata hivyo, huo si wito! Mungu huwa haiti namna hiyo. Bwana anapokuita kwenye jambo lolote lile ni kwa nia nzuri na kwa ubora na utukufu wake mwenyewe na si vinginevyo.

3) Kutafuta matakwa yako binafsi

Hii ni namna ambayo mwanadamu anaitumia kama mwamvuli kuendeleza mambo yake mengine kupitia utumishi jambo ambalo sio sahihi kabisa kama kutafuta umaarufu, jina kubwa na mengineyo.

*"Maana wengi huenenda, ambao nimewaambieni mara nyingi habari zao, na sasa nawaambia hata kwa machozi, kuwa ni adui za msalaba wa Kristo; 19mwisho wao ni uharibifu,* ***mungu wao ni tumbo****, utukufu wao u katika fedheha yao, waniao mambo ya duniani. 20Kwa maana sisi, wenyeji wetu uko mbinguni; kutoka huko*

*tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo;"* Wafilipi 3:19-20

Nimewekeza sura moja kufafanua swala hili kwenye kitabu cha **"Kazi ya Mungu ni Kazi"**. Kuna mitume wa uongo ambao waliingia kwenye utumishi ili kujipatia umaarufu, mapato ya udhalimu au kumpinga mtume Paulo. Ni vyema kujikagua na kuichunguza nia yako ya ndani.

4) Kukosa cha kufanya na kujificha kwenye kusema umeitika wito.

Tambua kwamba wito sio jambo la kuitika kama ziada. Utumishi ni jambo limebeba maisha yote kwa ujumla sasa kuitika kama jambo la ziada sio sahihi. Si mahali pa kukimbilia baada ya machaguo na fursa zingine zote kufunga.

Nilistaajabu baada ya kufanya *"desk review"* na kuona watu wengi walioitwa na Mungu waliitwa wakiwa kwenye kilele cha mafanikio yao; wakati kila kitu kinaenda sawa. Mpendwa, kushindwa maisha si ishara ya kwamba unaitwa!

# SURA YA SITA: MKAZO KUHUSU WITO (UTUMISHI)

Kuna mikazo minne ambayo ninapenda kuiwasilisha kwako kama mambo ya kuyapa umakinifu tunapozungumzia wito. Na kwa upande mwingine ni kama tahadhari kwa anyesikia kuitwa. Ni maeneo yanahitaji uangalifu kuyaangalia.

1. Wito ni wa kiungu. Asili yake ni Mungu na hivyo anayeita ni mwenye wito (Mungu). Usijaribu kulifanya swala la wito kuwa ni la kimwili. Hili ni swala la kiroho. Kwa hiyo, unaposikia wito unawaka ndani yako uelewe kwa miwani ya kiroho si kimwili.Watu wanaweza wasikuelewa, wasikubaliane na wewe, wakakupinga… ni sawa!

Nimefundisha jambo hili tena na tena ya kwamba vigezo vya kuita anavyo Mungu mwenyewe. Ajabu na kweli hakuita wenye hekima, wenye nguvu na wenye cheo wa dunia hii. Ili ijulikane ni Yeye mwenyewe anayetenda na siyo vigezo vyetu.

Nyakati unasikia moto mifupani mwako ni nyakati zako za mifungo binafsi, kusoma neno la Mungu, kusikiliza mafundisho, kusoma vitabu vya mafundisho, mikesha mingi… ni nyakati za kuingiza kazini nidhamu za kiroho ili kuuelewa na kuupokea wito.

Mpendwa wangu, usiuendee wito kieyeji au kimwili. Usikubali kuingia kwenye huo mtego. Hakikisha unausikia, unaupokea na unauelewa kwa jinsi ya kiroho.

2. Wito ni wa kiroho na sio kitaaluma wala vinginevyo.

Ninaomba niseme hapa kwa unyenyekevu wala si kwa kujivuna kwa sababu kile ninaenda kukifafanusha. Mimi nimepewa neema na Bwana Yesu ya kusoma elimu ya duniani na elimu ya Mungu (Theolojia) kwenye ngazi za ubobevu. Kwa hiyo, sitasema yafuatayo eti kwa vile sina taaluma.

Namna ya kwanza ya kuitikia wito si kwa kwenda kusomea. Namna ya kutambua ya kwamba umeitwa si kwa kwenda kusomea. Kumbuka huu ni wito wa kiroho.

Tunaitwa kuwa wahudumu wa injili ya Kristo kwenye maisha ya watu na si wadhahiri au wachambuzi. Huu ni mtego wa muda mrefu kwa kanisa, kwa maoni yangu. Wengine walienda kusoma ili wasikie wito; na wengine walienda kusoma ili waelewe wito… wakarudi wamepishana na majira na nyakati. Wakarudi na elimu, vyeti na vigezo vya kibinadamu tu.

Taaluma inaingia wapi? Linaweza kuwa swali la moyo wako. Ni hivi, ninashauri mtu aitike wito, atendee kazi, athibitike katika wito kisha aupeleke wito kujifunza (train the calling). Unaona utofauti? Ninachokaza hapa ni nini kinatangulia… kuitika na kuupokea wito kabla ya maswala ya taaluma.

3. Wito ni jambo binafsi, hivyo anayeweza kuelewa ni mtu binafsi.

Mungu huita mtu mmoja… mtu binafsi. Mungu hajawahi kuita watu kwa ngazi ya kundi au kwa hali ya upamoja. Mungu humchomoa mtu kutoka kwenye umati na kumleta mahali ambapo watazungumza peke yao- Mungu na mtu anayemuita.

*"BWANA akamwambia Musa, **Njoo huku juu kwangu mlimani, uwe huku**; nami nitakupa mbao za mawe na ile sheria na hiyo amri niliyoiandika ili uwafundishe."* Kutoka 24:12

Unaweza kujifunza kwa wengine… unaweza kuwatazama wengine kama kielelezo… unaweza kufuata mifano ya waliokutangulia. Lakini, tambua wito ni wa kibinafsi. Ruhusu Mungu akuchonge kwa namna yake ili kufaa kile anachokuitia.

Ni vyema kutambua ya kwamba wito huja na maisha na mtindo wa upweke na kujitenga. Anza kukubali na kuzoea jambo hilo.

4. Wito umefungamanishwa na kipimo cha muda, ukipita muda wako Bwana ataacha kuweka mzigo huo.

*"Malaika wa BWANA akamtokea, katika mwali wa moto uliotoka katikati ya kijiti; akatazama, na kumbe! Kile kijiti kiliwaka moto, nacho kijiti hakikuteketea.**Musa akasema, Nitageuka sasa,** niyaone maono haya*

*makubwa, na sababu kijiti hiki hakiteketei*." Kutoka 3:2-3

Wito huja na hai ya uharaka… udharula! Unataka uuitikie saa iyo hiyo. Wito si kitu cha kuahirisha na kusogezwa mbele. Kwa sababu Mungu anaenda na majira na nyakati alizojiwekea mwenyewe. Kwa hiyo, unapochelewa kuitika au kuelewa, au unapoashirisha… utashangaa siku moja huo mzigo utapotea moyoni.

*"Kwa hiyo, kama anenavyo Roho Mtakatifu, **Leo**, kama mtaisikia sauti yake, 8 Msifanye migumu mioyo yenu, Kama wakati wa kukasirisha,Siku ya kujaribiwa katika jangwa,"* Waebrania 3:7-8

*"hapo inenwapo, **Leo**, kama mtaisikia sauti yake, Msifanye migumu mioyo yenu, Kama wakati wa kukasirisha."* Waebrania 3:15

*"aweka tena siku fulani, akisema katika Daudi baada ya muda mwingi namna hii, **Leo**; kama ilivyonenwa tangu zamani, **Leo,** kama mtaisikia sauti yake, Msifanye migumu mioyo yenu."* Waebrania 4:7

Ninataka uone mkazo wa LEO! Unaisikia sauti leo, unaielewa na uinaiitikia.

# SURA YA SABA:

# VIZUIZI HIVYO NI KAMA

Kwenye sura hii nimekusudia kukusaidia kuvitambua vizuizi  na kuinuka juu yake ili visikuzuilie kuitika wito.

Hivi ni jumla ya vitu vyote ambavyo huinuka kama ukuta wa kuzuia kufika hatua ya kuitika kwenye wito ma vizuizi vyote hivi huja kama mtego na kwa nje vinaoneka ni sahihi lakini kunakua na mtego ndani yake juu ya kuitikia wito.

1. Umri

*"Ndipo niliposema, Aa, Bwana MUNGU! Tazama, siwezi kusema; maana mimi ni mtoto."* Yeremia 1:6

Yakupasha ushinde na kuinuka juu ya hiki kikwazo. Wanadamu wamejiwekea ukomo wa umri wa nani anaweza kufanya nini. Ninaweza kuwaelewa kutokea kwenye nia yao njema ya kwamba kwa ujumla, ukomavu huambatana na umri. Lakini sivyo ilivyo kwa Mungu. Anaweza kumuita yeyote anayemtaka kuja kwenye wito.

Kila jamii ina viwango ilivyojiwekea vya umri. Usikubali kuzuilika kwa kigezo cha umri kwa vipimo vya kijamii.

Kwenye jamii inaeleweka kabisa kwamba ianwezekana vijana:

- Kufanya migomo na ikawa ni hatari
- Kushiriki kwenye michezo kwa mafanikio makubwa
- Kushiriki siasa na kuleta matokeo
- Kujihusisha na shughuli za uhalifu na ugaidi na wakaleta madhara
- Kujihusisha na tabia za ngono na kuwa wazazi bila kupangilia (ndiyo maana wanawafundisha elimu ya afya uzazi na kuwashauri njia za kutumia)

Isipokuwa tu: Kumtumikia Mungu! Wanaonekana ni wadogo bado. Mpendwa wangu, usizuilike! Usikubali kutegwa hapo.

2. Tabia iliyozalishwa na ushirika

*"Ndipo niliposema, **Ole wangu! Kwa maana nimepotea;** kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu; na macho yangu yamemwona Mfalme, Bwana wa majeshi."* Isaya 6:5

Kutokea hapo utaona kwamba kujiona hufai haimaanishi Mungu hawezi kukuita hivyo utambuzi huo ukusukume kuelekea kwenye kuwa mtu bora kwa kuongeza utegemezi wako kwa Mungu. Ukweli ni kwamba Mungu haiti vitu bora, bali inavifanya kuwa bora vile alivyoviita.

3. Kujisikia duni

*"Musa akamwambia Mungu, Mimi ni nani, hata niende kwa Farao, nikawatoe wana wa Israeli watoke Misri?"* Kutoka 3:11

Kutokea hapo kuna dhana zinapaswa kuchotwa nazo ni kujiamini, kujikubali, kujithamini na kujielewa. Tambua kwamba watu maalum wametengwa kwa ajili ya wito.

Wewe si mtu wa hovyo. Mungu anakuona ni wa thamani machoni pake Yeye Mwenyewe ndiyo maana amekuita.

4. Kuukataa wito

*"Simoni Petro alipoona hayo, alianguka magotini pa Yesu, akisema, Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, Bwana."* Luka 5:8

Kumfukuza mwenye wito (BWANA) ni kufukuza wito wako, na kufukuza wito ni kufukuza uelekeo wa maisha kwa ujumla.

Kuna nyakati ambazo Mungu anajifunua kwa ukubwa ikilinganishwa na uwezo wako kumuelewa kiasi kwamba unaishia kukataa.

Shinda hicho kizuizi kwa kukubali ya kuwa Yeye ni Mungu.

**Kuhusu Mwandishi:**
Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

**Kuhusu New Vine Church:**
Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

## Mawasiliano na Mwandishi:



NEW VINE CHURCH | Dodoma



New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13 -14/Yoeli 2:2 - 11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



**Mahali tulipo:** Swaswa mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini.

## Ratiba za Ibada

**Alhamisi** Saa 11:15 jioni - saa 12:15 jioni
**Jumapili** Saa 3:00 asubuhi - saa 6:30 mchana

nvc_dodoma +255 754 917 764

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa BWANA na Mwokozi wa maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma


pastorjameskalekwa
+255 754 917 764
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
MchungajiJK
+255 754 917 764